

CHANGIA UJENZI.

Na Thadeo Mluge

Kwa hamasa!

1. Ka ni sa ni nyu mba ya Mu ngu cha ngi a, Li jengwe a ka e Mwe nye zi
8 1. cha ngi a, Na wa tu wa mu a bu di e cha ngi a Mu ngu a tu ku zwe.
15 Cha - ngi a ka ni sa a e cha ngi a u je nzi. cha ngi a kwa
Hi mi za na we ngi ne .wa la u si
20 fu ra ha a e cha ngi a u je nzi. a u je nzi wa KA NI SA.
zu i e

CHANGIA UJENZI

1. Kanisa ni nyumba ya Mungu changia,
Lijengwe akae Mwenyezi changia,
Na watu wamuabudie changia
Mungu atukuzwe.

*Changia kanisa ae changia ujenzi.
Changia kwa furaha ae changia ujenzi.
Himiza na wengine ae changia ujenzi.
Wala usizue ae changia ujenzi wa KANISAAAA...*

2. Ebu ndugu jifikirie changia,
Bahati uliyoipata changia,
Kujenga nyumba ya Mwenyezi changia,
Mungu atukuzwe.

3. Jitume kwanza we mwenyewe changia,
Waambie na ndugu zako changia,
Ijengwe nyumba ya Muumba changia,
Mungu atukuzwe.

4. Haya kinababa simama changia,
Nanyi kinamama nyanyuka changia,
Pia vijana na watoto changia,
Mungu atukuzwe.